



TAMKO LA KITUO CHA UWEKEZAJI LA KUKANUSHA KUHUSISHWA NA TANZANIA INVESTORS ASSOCIATION KATIKA TAARIFA ILİYOTOLEWA KATIKA MITANDAO

Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kilianzishwa na Sheria ya Bunge Na. 26 ya mwaka 1997. Malengo ya kuanzishwa TIC pamoja na mambo mengine ni kuwa taasisi mama ya Serikali ya Tanzania yenye lengo kubwa la kuratibu, kuhimiza, kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji Tanzania na kuishauri Serikali kuhusu sera ya uwekezaji na mambo mengine yote yanayohusu uwekezaji nchini. Majukumu ya Kituo cha Uwekezaji yameainishwa na kufafanuliwa vizuri katika Kifungu cha 5 cha Sheria ya Uwekezaji Tanzania Sura ya 38.

Katika kutekeleza majukumu yake, Kituo kinafanya kazi na wadau (wazawa na watu kutoka nje ya nchi) ili kuweza kukuza uwekezaji endelevu utakao ongeza ajira na mapato kwa nchi kupitia kodi na kukuza sekta binafsi.

Siku za hivi karibuni, Kituo cha Uwekezaji kimekua kikipigiwa simu na watu wa kada mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kuhusu taarifa zilizosambaa mitandaoni zikihusisha Kituo cha Uwekezaji na wanaojiita Umoja wa Wawekezaji Tanzania (Tanzania Investors Association) zikimlenga Bw. Abdulsamad Abdulrahim.

Kituo cha Uwekezaji Tanzania kinapenda kutoa Tamko rasmi la **kukanusha kuhusika na "Tanzania Investors Association"**. TIC haihusiki na chochote kilichoandikwa katika taarifa hiyo iliyotolewa na wanaojiita "Tanzania Investors Association". Pia TIC haiitambui "Tanzania Investors Association" na washirika wake.


Aidha, Kituo kinapenda kukanusha kuhusu uwepo wa kitengo cha "Investor Protection Unit" kama kilivyotajwa katika taarifa husika, Kitengo hiki hakipo na kwamba Muhusika anayeshughulika na kitengo kilichotajwa kuwa ni Bw. David Siwa, Kituo cha Uwekezaji kinapenda kukanusha kuwa Bw. David Siwa, siyo mtumishi wa Kituo cha Uwekezaji, na kituo hakijawahi kuwa na mtumishi mwenye jina hilo, hivyo, taarifa hizo ni za uongo.

Kwa tamko hili tunaomba ifahamike kwa wadau wote wa uwekezaji kutoka sekta ya umma na binafsi, ndani na nje ya nchi kuwa TIC haihusiki wala haitambui taarifa hiyo. Na Kituo kinashauri wadau wote wanaoitakia mema nchi yetu, tuendeleo kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na kama kuna tatizo lolote kuhusu uwekezaji liwasilishwe kwenye mamlaka husika, na sio kutoa matamko kama haya kwa kujificha bila kujua chanzo /chimbuko la tamko hilo.

Kwa upande wa Bw. Abdulsamad Abdulrahim, Kituo kinamtambua kama mdau muhimu katika kukuza sekta binafsi na amekuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na Serikali katika masuala mazima ya Mafuta, Petroli na sekta zingine. Aidha, Bw. Abdulsamad Abdulrahim ni Mwanzilishi na Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watoa Huduma za Mafuta na Gesi Tanzania (ATOGS) na vile vile ni mjumbe wa bodi ya TPSF ambapo tunafanya kazi kwa karibu sana na TPSF na pia tunatambua Ubalozzi wake wa Heshima kwa nchi ya Brazil hapa nchini kwa upande wa Zanzibar.

Kupitia taarifa hii ieleweke kuwa wadau wote wanaosaidiana na Serikali na kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhamasisha uwekezaji nchini bila kuvunja sheria, Kituo cha Uwekezaji, tutaendelea kushirikiana nao.

IMETOLEWA NA
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA

SAHIHI: .....
TAREHE: 01-11-2018.....